

HATI YA KUPAMBANA NA UBAGUZI WA RANGI YA KIKUNDI CHA BENKI YA DUNIA

KANUNI SEPTEMBER 2021

KANUNI YA

1

Kikundi cha Benki ya Dunia kimejitolea kutovumilia hata kidogo ubaguzi wa rangi na ubaguzi wa kimbari katika njia na muktadha wote.

KANUNI YA

2

Kukabiliana na ubaguzi wa rangi na ubaguzi wa kimbari katika njia na muktadha wote katika taasisi ni muhimu katika kufanikisha malengo mawili ya Kikundi cha Benki ya Dunia ya kuondoa uchochole na kuhamasisha ustawi unaoshirikiwa.

KANUNI YA

3

Kikundi cha Benki ya Dunia kimejitolea kupambana na ubaguzi wa rangi na ubaguzi wa kimbari na kukuza usawa na haki kwa wote kwa kujali shirika na usimamizi wake, ikijumuisha katika kufanya uamuzi kuhusu uajiri na ukuzaji wa talanta.

KANUNI YA

4

Kikundi cha Benki ya Dunia kinatafuta kukuza ujumuishaji wa wote na kukabiliana na ubaguzi wa rangi na ubaguzi wa kimbari kupitia miradi, mipango na uwekezaji ambao kinafadhili ili kufanikiwa kukabiliana na changamoto za maendeleo na kuleta maendeleo endelevu.

KANUNI YA

5

Kikundi cha Benki ya Dunia kinatafuta kuleta ujumuishaji na kupambana na ubaguzi wa rangi katika jamii ambamo tunaishi na kufanyia kazi kupitia uhusiano wa jamii wenye ufanisi.

KANUNI YA

6

Kikundi cha Benki ya Dunia kinatambua kwamba ubaguzi wa rangi na ubaguzi wa kimbari unashutumiwa kimaadili, ni kinyume cha Itikadi zetu za Msingi, na si halali chini ya sheria ya kimataifa na sheria za nchi kadhaa wanachama wake.



WORLD BANK GROUP